

KISWAHILI NA MAENDELEO YA KIJAMII

UCHANGANYAJI WA LUGHA KATIKA JAMII YA WAZANZIBARI: MFANO KUTOKANA NA WILAYA YA MJINI NA MAGHARIBI UNGUJA, ZANZIBAR.

Zahor Mwalim Muhidin
Chuo Kikuu cha Zanzibar
zamwa2013@yahoo.com

Ikisiri

Wazanzibari hupenda kuchanganya lugha. Mara nyingi, wao huchanganya lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu. Mtindo huu unaweza kuthibitishwa kihistoria kutokana na athari ya mchanganyiko wa Waswahili wa Zanzibar na wageni wa Kiarabu kabla, wakati na baada ya ukoloni; pamoja na majilio ya wageni wa kizungu wakati na baada ya ukoloni (Broomfield, 1931; Krapf, 1878; na Topan, 1992). Athari hizi ziligundulikana katika tafsiri za awali zilizofanyika Zanzibar. Tafsiri hizi zilibainisha kuwa lugha ya Kiswahili imeathiriwa kwa kiwango kikubwa na lugha ya Kiarabu kwa kukopa maneno mengi ya Kiarabu ya dini ya Uislamu pamoja na maneno mengine kutokana na lugha ya Kiingereza. Kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni hadi leo, Wazanzibari wengi huanza elimu ya msingi katika madrasa za dini ya Uislamu kabla ya kuingia katika skuli za kawaida. Kutokana na misingi hiyo, watoto wengi huathiriwa na lugha ya Kiarabu na lugha ya Kiingereza. Wanapofikia katika rika la ujana, kila mmoja huwa ameathirika kutokana na muelekeo wa jinsi anavyotaka athaminiwe na jamii. Kutokana na hali hii, kuna mtindo wa kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu katika mazungumzo ya kawaida au wakati wa kupata au kutoa mafunzo ya dini ya Uislamu. Katika kufanya hivi, vijana hawa hupata uso katika jamii kuwa ni ustadhi au shekhe katika elimu na mafunzo mema ya dini ya Uislamu. Wengi wao hubakia na sifa hiyo mpaka umri wa utuuzima. Kwa wale wanaochanganya Kiswahili na Kiingereza, kwa upande mwingine huwa na nia ya kuonekana kama wasomi. Pamoja na hawa walio na ujuzi wa Kiingereza, kuna wengine wanaojinasibisha nao japo hawana ujuzi wa kutosha wa Kiingereza. Vijana hao wameibua mtindo ama rejista ijulikanayo kama lugha ya vijana. Ni mitindo hii ya uchanganyaji wa lugha itakayozingatiwa katika makala hii kama inavyojitokeza miongoni mwa jamii ya Wazanzibari.